

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
United Republic of Tanzania

WIZARA YA MADINI
Ministry of Minerals

TUME YA MADINI
The Mining Commission



TAARIFA KWA UMMA
Public Notice

Tume ya Madini Iliundwa kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha Sheria ya Marekebisho Anuwai ya Sheriaya Madini Na. 7 ya Mwaka 2017. Mnamo tarehe 17 Aprili, 2018, Mhe. Rais wa Jamhuriya Muunganowa Tanzania, Dr. John Pombe Joseph Magufuli, kulingana na Sheria tajwa, aliteua Mwenyekiti na Makamishna wa Tumeya Madini. Ili kutekeleza majukumu yake, Tume ilifanya kikao chake cha kwanza tarehe 30 Aprili, 2018 Jijini Dodoma. Pamoja na mambo mengine, Tume iliazimia mambo yafuatayo:

The Mining Commission was established in accordance with Section 21 of the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 7 of 2017. On 17 April 2018, Hon. President of the United Republic of Tanzania, Dr. John Pombe Joseph Magufuli, appointed the Chairman and Commissioners for the Mining Commission in accordance to the mentioned Act. In order to carry out its obligations, the Commission held its first session on 30 April 2018 in Dodoma. Among other things, the Commission resolved the following:

1. Ofisi za Makao Makuu ya Tume ya Madini zitakuwa Jijini Dodoma katika Ofisi za Wizara ya Madini;

The head quarters for the Mining Commission will be located in Dodoma at the offices of Ministry of Minerals;

2. Kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake ya Mwaka 2017 kwa lengo la kuhakikisha kuwa Serikali inamiliki hisa zisizopungua asilimia 16 ya mtaji wa Kampuni zinazomiliki migodi ya kati (MLs) na mikubwa (SMLs), Wazawa wanashirikishwa ipasavyo katika Miradi ya Madini na kunufaisha jamii katika maeneo ya migodi na Taifa kwa ujumla;

Strengthening the management of the 2010 Mining Act and its 2017 amendments with an aim of ensuring that the Government owns not less than 16% of the shares in the capital of companies holding Mining Licences (MLs) and Special Mining Licences (SMLs), and the nationals are involved accordingly in the Mining Projects and to benefit communities in mining areas and the nation at large;

3. Kuwajulisha wamiliki wote wa leseni zote za kuhodhi maeneo (Retention Licences – Jedwali Na. 1) kuwa leseni zao zimefutwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017 na Kanuni ya 21 ya Kanuni za Madini (Haki Madini), 2018 Tangazo la Serikali Na. 1 / 2018 na kwamba maeneo ya leseni hizo yamerudishwa Serikalini bila hakikisho la kupewa tena;

Notifying all holders of Retention Licenses – (Table No. 1), that their licenses have been cancelled pursuant to the Mining Act 2010 read together with its amendments of 2017 and regulation 21 of the Mining (Mineral Rights) Regulations, 2018 GN No. 1/2018 and that areas where such licenses were granted have been returned to the Government without a re-issue warranty;

Jedwali Na. 1: Orodha ya leseni za kuhodhi maeneo zilizofutwa
Table No. 1: List of Retention Licenses, which have been cancelled

Namba ya Leseni	License Number
Jina la Mmiliki	Name of Holder
Aina ya Madini	Mineral Type
Tarehe ya kutolewa	Issue date
Tarehe ya kuisha	Expiry date
Ukubwa (Km)	Size (Km)
Mkoa / Wilaya	Region / District
Hali halisi	Current Status
Imefutwa	Cancelled

Namba ya Leseni	Jina la Mmiliki	Aina ya Madini	Tarehe ya kutolewa	Tarehe ya kuisha	Ukubwa (Km ²)	Mkoa/Wilaya	Hali halisi
RL 0001/2009	Kabanga Nickel Company Limited	Nickel	02/05/2009	01/05/2019	201.85	Kagera/ Ngara	Imefutwa
RL 0006/2009	National Mineral Development Corporation Limited	Gold	31/12/2009	30/12/2019	21.27	Shinyanga/ Kahama	Imefutwa
RL 0009/2014	Bafex Tanzania Limited	Silver, gold & Copper	01/09/2014	31/08/2019	12.58	Mbeya/ Chunya	Imefutwa
RL 0010/2014	Bafex Tanzania Limited	Silver, gold & Copper	01/09/2014	31/08/2019	12.59	Mbeya/ Chunya	Imefutwa
RL 0011/2014	Bafex Tanzania Limited	Silver, gold & Copper	01/09/2014	31/08/2019	11.83	Mbeya/ Chunya	Imefutwa
RL 0012/2014	Bafex Tanzania Limited	Silver, gold & Copper	24/09/2014	23/09/2019	11.27	Mbeya/ Chunya	Imefutwa
RL 0014/2014	Mabangu Mining Limited	Gold	31/10/2014	30/10/2019	2.94	Geita/Mbogwe	Imefutwa
RL 0015/2014	Resolute (Tanzania) Limited	Gold	31/10/2014	30/10/2019	0.91	Geita/Mbogwe	Imefutwa
RL 0016/2015	Wigu Hill Mining Company Limited	Rare Earth Elements	13/02/2015	12/02/2020	15.14	Morogoro	Imefutwa
RL 0017/2015	Nachingwea Nickel Limited	Nickel	21/04/2015	20/04/2020	48.8	Lindi /Nachingwea	Imefutwa
RL 0013/2014	Precious Metals Refinery Company Limited	Nickel	10/10/2014	09/10/2019	25.7	Simiyu/ Bariadi & Busega	Imefutwa

4. Hadi kufikia tarehe 04/07/2017, kulikuwa na jumla ya maombi mapya ya leseni za uchimbaji wa kati (MLs) zipatazo 15 na ya kuhuisha 21. Pia maombi ya leseni za uchimbaji mdogo wa madini (PMLs) yalikuwa 4,345 katika Ofisi za Madini za Mikoa na Wilaya kote nchini. Kadhalika, hadi kufikia tarehe 04/07/2017, kulikuwa na jumla ya maombi 240 ya leseni za utafutaji wa madini (PLs). Kati ya maombi hayo, 86 yalishalipiwa ada ya kuandalia leseni (preparation fee) na yaliyobaki hayajalipiwa. Kwa taarifahi, waombaji wote wa leseni za madini wanatakiwa kukamilisha maombi yao ili yaendane na matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2017. Hi ni pamoja na:

Until 4 July 2017, there were a total of 15 new applications for Mining Licences (MLs) and 21 renewals. Also there were 4,345 applications for Primary Mining Licences (PMLs) at regional and district mining offices throughout the country. Likewise, until 4 July 2017, there were 240 applications for Prospecting Licences (PLs). Among the said applications, preparation fees were paid for 86 applications and the rest were not paid for. With this information, all mineral licensing applicants are required to complete their application in order to comply with the requirements of the 2010 Mining Act as amended in 2017, which includes:

- a. Kulipia ada za kuandalia leseni za madini (PLs, PMLs, MLs na SMLs) kwa maombi yaliyokidhi vigezo vya kupewa leseni;

Paying for mineral licence preparation fees (PLs, PMLs, MLs and SMLs) for applications that have complied with the licensing conditions;

- b. Kuwasilisha Local Content Plan kwa mujibu wa Vifungu vya 102, 103 na 104 vya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho Anuwai ya Sheria zilizoandikwa, Sheria Na. 7 ya Mwaka 2017; kwa waombaji wa leseni za uchimbaji wa kati (MLs) na mkubwa (SMLs) wa madini;

Submitting Local Content Plan in accordance with Sections 102, 103 and 104 of the Mining Act 2010 as amended by the Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act No. 7 of 2017 for applicants of Mining Licences (MLs) and Special Mining Licences (SMLs);

- c. Kuwasilisha Corporate Social Responsibility Plan; na tamko la Integrity Pledge kadri ya kifungu cha 105 na 106 kwa mtiririko huo wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2017 kwa waombaji wa leseni za uchimbaji wa kati (MLs) na mkubwa (SMLs) wamadini;

Submitting Corporate Social Responsibility Plan, with the declaration of Integrity Pledge as contemplated in sections 105 and 106 respectively of Mining Act 2010 as amended by the Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act No. 7 of 2017 for applicants of Mining Licences (MLs) and Special Mining Licences (SMLs);

- d. Waombaji wote wa leseni za utafutaji wa madini (PLs) kuwasilisha taarifa za technical resources (Mine equipment, technical personnel, ...) na Audited Financial Statements;

All applicants for Prospecting Licences (PLs) to submit a report on technical resources (Mine equipment, technical personnel, ...) and Audited Financial Statements;

- e. Waombaji wote wa leseni za uchimbaji wa kati (MLs) na mkubwa (SMLs) kuwasilisha Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira (Environmental

Impact Assessment – EIA Certificate), taarifa za Feasibility Studies, technical resources (Mine equipment, technical personnel, ...), Audited Financial Statements, uthibitisho wa tathmini ya fidia na kutokuwepo kwa mgogoro / migogoro katika eneo linaloombewa leseni ya uchimbaji wa madini; na

All applicants for Mining Licences (MLs) and Special Mining Licences (SMLs) to submit the Environmental Impact Assessment Certificate (EIA Certificate), Feasibility Studies, technical resources (Mine equipment, technical personnel, ...), Audited Financial Statements, proof of compensation assessment and absence of conflicts / conflicts in the area where the application for mining licence has been made; and

- f. Waombaji wote wa leseni za uchimbaji mdogo wa madini (PMLs), baada ya kupata leseni na kabla ya kuanza shughuli za uchimbaji, wawasilishe Mpango wa Uhifadhi wa Mazingira (Environmental Protection Plan – EPP);

All applicants for Primary Mining Licence (PMLs), after obtaining licenses and before starting extraction activities, should submit Environmental Protection Plan (EPP);

Nyaraka zote zinazotakiwa, ziidhinishwe na mamlaka zinazohusika na kuwasilishwa kwa Mtendaji Mkuu wa Tume ya Madini kupitia Sanduku la Posta 2292, DODOMA.

All documents required have to be approved by all relevant authorities and submitted to Chief Executive Officer of the Commission via Postal Box 2292, DODOMA.

Imetolewa
Issued by:

na:

Prof.
MWENYEKITI
Chairman
Mei
11 May 2018

Idris

11,

Kikula

2018